

## **HALMASHAURI YA WILAYA YA CHEMBA**



**FURSA ZA UWEKEZAJI KATIKA ENEO LA**  
**MIFUGO KATIKA KIJIJI CHA KELEMA MASHARIKI**

## **1.0 Utangulizi**

Eneo la Mifugo la Kelema Mashariki lilianzishwa mwaka **1954** na utawala wa kikoloni wa Mwingereza kwa ajili ya kuanzisha kituo cha kupumzisha Mifugo na kuchanja kabla ya kusafirishwa na kuuzwa kwenye masoko ya Mifugo. Baada ya Uhuru wa Tanganyika ,(Kelema Animal Holding Ground) ilichukuliwa na Wizara ya Mifugo chini ya Tanzania Livestock Marketing Project (TLMP) ambayo ilikuwa ikinunua mifugo iliyokuwa ikichanjwa kabla ya kusafirishwa kwenda kiwanda cha Usindikaji nyama-Tanganyika Parkers, Dar Es Salaam.

Utambuzi wa mipaka pamoja na upimaji ulifanywa na Halmashauri ya Wilaya ya Chemba ambapo eneo hili lina ukubwa wa **ekari 1414.602** sawa na **hekta 565.8408**.

## **2.0 Miundo mbinu iliyopo**

Miundo mbinu wezeshi iliyoko ndani ya eneo la kituo cha Mifugo ni joshu na Kisima cha Maji ambacho kilichimbwa wakati wa uanzishwaji wa Mradi huo isipokuwa hakina pampu. Miundo mbinu hiyo inahitaji ukarabati wa kawaida ili kuendelea kufanya kazi tarajiwa. Josho lililopo lina ujazo wa litu 13,000 za maji.

## **3.0 Fursa zilizopo**

Baadhi ya fursa zilizopo kulingana na uwepo wa eneo hili ni kama ifuatavyo;

- E neo la ukubwa wa ekari 1414.6.
- Idadi kubwa ya mifugo katika Wilaya takribani ng'ombe 300,000,mbuzi 210,00,kondoo 180,000,kuku wa kienyeji 352000 na punda 12,000.
- Uzalishaji wa Mazao: (Alizeti tani 8,500), (Karanga tani 300), (Ufuta tani 1200), (Mbaazi tani 500), (Mahindi tani 24,000) na (Muhogo tani 200).
- Urahisi wa upatikanaji wa maji kutoka ardhini
- Urahisi wa upatikanaji wa huduma ya umeme
- Uwepo wa miundombinu ya barabara ya lami (Dodoma-Babati)
- Upatikanaji wa vibarua kwa wingi

## **4.0 Shughuli za kiuchumi zinazoweza kufanya katika eneo husika**

- Uanzishwaji wa viwanda kama vile kiwanda cha kuchakata nyama, kuzalisha vyakula vya mifugo.
- Uanzishwaji wa kiwanda cha kutengeneza mafuta ya alizeti.
- Kilimo na usindikaji wa mazao (Mahindi, Muhogo, ,Mbaazi, Ufuta na Karanga),
- Kilimo na usindikaji wa matunda na mbogamboga hasa kwa kutumia teknolojia ya (Greenhouse).
- Ufugaji wa Samaki kwa kuzuia mto au kuchimba visima na mabwawa (Aquaculture).
- Uanzishwaji wa kiwanda cha ngozi.
- Uanzishwaji wa mashamba ya malisho (Pasture land).

- Uanzishaji wa soko la mazao.

## **5.0 Changamoto**

- Changamoto kubwa iliyopo katika uendelezaji wa eneo husika:
- Ukosefu wa rasilimali fedha kwa ajili ya uwekezaji.

**Simon N. Langoi**

Afisa Mifugo na Uvuvi (H/W)

**CHEMBA**